JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya simu. **SHULE YA SEKONDARI SWAYA.**
Simu. 0753004401 **S.L.P 2091,**
E-mail: swaya sec @gmail.mail **MBEYA.**

7/12/2020

Unapojibu tafadhari taja.
Kumb.Na. MDC/SWY/2020/……

Kwa
……..
……..
…….

YAH: MASHARTI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SWAYA.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Swaya kidato cha kwanza kuanzia Januari 2021. Shule ya Sekondari Swaya ipo Mbeya vijijini kilomita zipatazo 9 toka stendi kuu ya mabasi ya Mbeya jiji. Ukifika stendi kuu, panda daladala za Mbalizi au Iyunga. Shuka kituo cha Iyunga, hapo utapanda pikipiki (nauli tshs. 2,000/=) umbali wa kilomita 5 hadi shuleni Swaya.

Shule itafunguliwa rasmi tarehe 04/01/2021 Saa 2:00 asubuhi. Unatakiwa kuripoti tarehe hiyo bila kukosa.

Mambo muhimu ya kuzingatiwa yameambatanishwa pamoja na barua hii.

Hongera na KARIBU SANA Shule ya Sekondari Swaya.

……
MAIKO H. SWILLA
MKUU WA SHULE.
0753004401

Nakala: Katibu Mtendaji,
Wizara ya OR-TAMISEMI,
S L P 9121,
DAR –ES-SALAAM.

Afisa elimu mkoa,
S.L.P 756 – MBEYA.

Mkurugenzi mtendaji(w),
Halmashauri ya wilaya ya Mbeya,
S.L.P. 599,
MBEYA.

Afisa elimu sekondari(w),
Halmashauri ya wilaya ya Mbeya,
S.L.P 599,
MBEYA.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. **SARE ZA SHULE**

   A. **WAVULANA**
      I. **SURUALI MBILI (2) RANGI YA KAKI ESTEEM NAMBA 1(turn up), CELEBRATION MBILI NA MKANDA MWEUSI WA NGOZI (MODAL AU SURUALI ZINAZOBANA HAZIRUHUSIWI).**
      II. **MASHATI MAWILI MEUPE (tetroni) MIKONO MIFUPI YENYE UREFU WA KUTOSHA KUCHOMEKEWA NDANI YA SURUALI.**
      III. **JOZI MBILI (2) ZA VIATU VYA NGOZI VYA KUFUNIKA NA KAMBA NA VISIWE NA VISIGINO VIREFU.**
      IV. **JOZI MBILI (2) ZA SOKSI NYEUSI KWA WAVULANA TU.**
      V. **SWETA RANGI YA DAMU YA MZEE MIKONO MIREFU.**

   B. **WASICHANA.**
      I. **SKETI MBILI (2) RANGI YA KAKI ESTEEM NAMBA 1 ZENYE UREFU UNAOFIKA KWENYE KIWIKO CHA UNYAYO MARINDA UPANA WA VIDOLE VITATU(sketi fupi na modal haziruhusiwi).**
      II. **MASHATI MAWILI MEUPE (tetroni) MIKONO MIFUPI YENYE UREFU WA KUTOSHA KUCHOMEKEWA NDANI YA SKETI .**
      III. **JOZI MBILI (2) ZA VIATU VYA NGOZI VYA KUFUNIKA NA KAMBA NA VISIWE NA VISIGINO VIREFU.**
      IV. **JOZI MBILI (2) ZA SOKSI NYEUPE KWA WASICHANA TU.**
      V. **SWETA RANGI YA DAMU YA MZEE MIKONO MIREFU.**

2. **VIFAA VYA DARASANI.**
      I. **BEGI LA KUBEBEA MADAFTARI**
      II. **MADAFTARI KUMI MADOGO A4 KWA AJILI YA ORIENTATION COURSE (BASE LINE COURSE), AMBAYO UTASOMA WIKI 6 ZA MWANZO, NA DAFTARI 11 COUNETR BOOKS KUANZIA QUIRE TWO(2) HADI QUIRE FOUR (4) KWA AJILI YA MASOMO YA KAWAIDA.**
      III. **KALAMU YA WINO NYEUSI AU BLUE PAMOJA NA PENSELI.**
      IV. **MKEBE WENYE VIFAA VYOTE (MATHEMATICAL SET).**

3. **VIFAA VYA MICHEZO.**
      I. **TRACKSUIT RANGI NYEUSI KWA WOTE.**
      II. **RABA YA MICHEZO KWA WOTE**

4. **VIFAA VINGINE:**
      I. **NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA.**
      II. **FAIL KWA AJILI YA KUTUNZIA KUMBUKUMBU ZA MWANAFUNZI.**

FOMU ZIFUATAZO ZIMEAMBATANISHWA:

A. **Medical examination form, ambayoinajazwa na daktari katika kituo cha afya cha serikali.**
B. **Fomu ya uthibitisho wa uraia, ambayo itajazwa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika wilaya atokako.(kwa asiye na nakala ya cheti cha kuzaliwa)**
C. **Fomu ya sheria na kanuni za shule, ambazo unatakiwa kuzisoma kwa makini na kuzielewa.**
D. **Fomu ya kukubali mwanafunzi na mzazi/ mlezi kufuata maelekezo na taratibu za shule.**

Fomu ya medical examination na fomu ya uthibitisho wa uraia zinatakiwa kurudishwa ofisi ya mkuu wa shule mara tu unapokamilisha kuzijaza (kabla au siku ya kufungua shule).

Fomu na. D hapo juu inayohusu kukubali mwanafunzi na mzaza/mlezi itajaziwa shuleni siku ya kufungua shule

ANGALIZO MUHIMU:

I. **Siku ya kufungua shule mwanafunzi anatakiwa kuja na mzazi/mlezi bila kukosa.**
II. **Mwanafunzi aje na vifaa vyote vilivyoainishwa hapo juu ikiwa ni pamoja na sare za shule. Kinyume na hapo mtoto wako hatapokelewa.**

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA KWA KIJANA WAKO.

……
MKUU WA SHULE.
0753004401

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

1. **Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.**
   Inatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti.
   a) **Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.**
   b) **Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.**
   c) **Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).**
   d) **Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.**
   e) **Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.**
   f) **Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.**
   g) **Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.**
   h) **Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.**

2. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule:**
   a) **Wizi.**
   b) **Uasherati, ubakaji na ushoga.**
   c) **Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.**
   d) **Uvutaji sigara, tumbaku na bangi.**
   e) **Makosa ya jinai.**
   f) **Kupigana au kupiga.**
   g) **Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.**
   h) **Kudharau bendera ya taifa.**
   i) **Kuoa au kuolewa.**
   j) **Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.**
   k) **Kutoa mimba.**
   l) **Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.**
   m) **Kukataa adhabu kwa makusudi.**

TAFADHARI SOMA KWA UMAKINI KANUNI ,SHERIA NA KANUNI HIZI.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

MKUU WA SHULE

O753 004 401

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
SWAYA SECONDARY SCHOOL.
BOX 2091,
MBEYA.

Date :…….

THE MEDICAL OFFICER,
…….
…….

PART "A"

Mr./ Miss (pupils name)…….……

Please examine the above named pupil as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories:

1. **Hemoglobin.**
2. **P.V. Bleeding.**
3. **Sight.**
4. **Blood pressure.**
5. **Urine for sugar and pregnancy test.**
6. **Stool for routine examination.**
7. **Asthma.**
8. **Skin disease.**
9. **Leprosy.**
10. **Any deformity.**
11. **Epilepsy.**
12. **Pulmonary tuberculosis.**
13. **Neurosis.**
14. **Venereal diseases.**
15. **Other serious diseases.**

PART "B"
MEDICAL CERTIFICATE.
(To be completed by a Government Medical Officer)

I (full names)……. A medical officer at …….. (name of hospital). I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full schooling.

Other comments: ……...
……..
……..

Date …….. **Signature and Stamp ……..**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FOMU YA KUKUBALI MWANAFUNZI NA MZAZI/ MLEZI

SEHEMU YA KWANZA

(ijazwe na mwanafunzi)

Mimi (majina kamili)……. nimekubali kujiunga kidato cha…… katika shule ya sekondari Swaya. Naahidi kuwa nitafuata na kutii kanuni, sheria na taratibu zote kama zilivyoelekezwa. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea (EK).

SAHIHI …… TAREHE ……

SEHEMU YA PILI

(ijazwe na mzazi)

Mimi (majina kamili) ……..mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, naahidi kuwa siku zote nitashirikiana na walimu kuhakikisha mtoto anapata elimu kama inavyotakiwa. Pia nitatimiza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na huduma kwa mwanafunzi kama ninavyotakiwa kufanya nikiwa kama mzazi. Kwa kipindi chote atakachokuwa shuleni.

SAHIHI …… TAREHE ……

NUKUU MUHIMU:

KUTOKUTEKELEZA HIKI ULICHOAHIDI HAPO JUU NI KUKIUKA TARATIBU ZA SHULE, HIVO HATUA ZA KINIDHAMU ZITACHUKULIWA DHIDI YA MHUSIKA.

SAHIHI YA MKUU WA SHULE

…….